



Siku za
16 Uanaharakati
2025
Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia

Kauli Mbiu: Fikiria Upya Mustakabali wa Kifeministi: Kuimarisha Mshikamano, kustawi baada ya Migogoro.

Mwongozo wa Shughuli za Kampeni ya mwaka 2025

1. Utangulizi

Mwaka huu, sio tu tunasimama kidete dhidi ya upinzani--bali katika mshikamano, matumaini, na fikra dhabiti. Mwaka wa 2025 katika Siku 16 za Uanaharakati zinatutaka kutafakari upya mustakabali wa ufeministi tunaostahili, ambao tutaishi maisha ya haki, na sio kuidai; ambapo uponyaji unapewa kipaumbele, na si kuahirishwa; na ambapo jamii ni msingi wetu, si mawazo ya baadaye. Hata hivyo, hatuwezi kufikiria tena bila kuzingatia. Duniani kote, harakati zinazotekelezwa za kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake zinakabiliwa na upungufu wa ufadhili kwa kiwango kikubwa, kupungua kwa nafasi za raia na vitisho vinavyoongezeka—hasa mtandaoni.

Ukatili unaohamasishwa kidijitali kwa njia ya uhalifu mtandaoni, kutoa taarifa ya kugushi kwa njia kutumia akili mnemba, ufuatiliaji na kumchimba mtu, imekuwa hali halisi ya kila siku kwa wanawake, wasichana, watu wa jinsia tofauti na wanaharakati. Haya si mashambulizi ya mtandaoni tu, ni mashambulizi ya kweli, yenye athari za kudumu kwa usalama, afya ya akili, na ushiriki katika umma.

Wakati huo huo, mipango mahususi inayowalinda waathirika, maeneo salama yenye rasilimali, kutoa ufadhili kwaajili ya nyumba salama, na ufadhili wa huduma za mkoba kwa jamii haupo au umesambaratishwa. Madhara ya kutochukua hatua hubebwa na wale ambao tayari wako hatarini zaidi.

Kampeni ya mwaka huu inatoa wito wa kuchukua hatua, ndiyo—halikadhalika inatoa ombi la dharura: inatukumbusha: mustakabali unaostahili kuuzingatia unahitaji **maono** na **rasilimali**.





2. Madhumuni ya Mwongozo wa Shughuli ya Kampeni

Madhumuni ya Mwongozo huu wa Shughuli za Kampeni ni kutoa mfumo unaoeleweka na unaotekelezeka kwa vitendo kwa ajili ya mashirika, wanaharakati, na wadau wanaoshiriki katika **kampeni ya mwaka 2025 ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia** chini ya kauli mbiu “ *Fikiria Upya Mustakabali wa Kifeministi: Kuimarisha Mshikamano, kustawi baada ya Migogoro .*”

Mwongozo huu unalenga:

1. **Kukuza uwiano na uelewa wa pamoja** - unaowaleta kwa pamoja wahusika wa kampeni katika dhamira moja, kuhakikisha kwamba juhudi zote zinazingatia kauli mbiu, ujumbe muhimu, na amali za ufeministi katika kiini cha kampeni.
2. **Msaada ulioratibiwa na kuchukua hatua kwa pamoja** - Itatumika kama zana ya kupanga, ushirikiano, na kuoanisha shughuli katika ngazi ya nchi, kimataifa na kikanda ili kuimarisha sauti ya pamoja na kuleta matokeo.
3. **Toa mawazo yanayo tekelezeka na zana** -Toa sampuli za shughuli, nyenzo za mawasiliano, na mbinu za utetezi ambazo zinaweza kutumika katika muktadha na hadhira tofauti.
4. **Hakikisha uthabiti katika utumaji wa ujumbe** - Inaongoza wadau jinsi ya kuwasilisha ujumbe wa kampeni kwa uwazi na kwa nguvu ili kuendeleza mshikamano, kujijali binafsi na kwa pamoja na kuleta mabadiliko ya kina.

3. Mikakati ya Kampeni

Mikakati ya mtandaoni ya ana kwa ana inapaswa kuzingatia amali za ufeministi, kuchukua hatua za pamoja, ubunifu, na ustahimilivu katika muktadha wa kupungua kwa nafasi unaochagizwa na migogoro. Hii itajumuisha; uhamasishaji wa pamoja na kujenga mshikamano, simulizi za hadithi za kifeministi na uanaharakati wa kidijitali, ushiriki wa vitendo unaoongozwa na jamii, utetezi, na ushawishi wa sera.

Mwaka huu kiti ya kuchukua hatua na Utetezi:

1. Utepe (Zambarau/Mweupe)
2. Mabango
3. Vipande vya Kuanzisha Majadiliano
4. Kadi za Uthibitisho
5. Sumaku za kubandika kwenye Jokofu.

Zaidi ya hayo, kalenda ya mezani ya mwaka 2026 imejumuishwa katika kiti yakuchukua hatua na utetezi ili kupanua tafakari, na uchunguzi zaidi katika kipindi cha kampeni ya mwaka huu hadi mwaka ujao.

Tumia nyenzo hizi kuibua tafakari, kuimarisha mazungumzo, na kuchagiza kuchukua hatua nyumbani kwako, shule, mahali pa kazi na katika jamii.





4. Jikite kwenye Kampeni

Kabla ya kuchukua hatua yoyote, pata muda wa kuelewa ujumbe na ari ya kampeni. Nyaraka za muongozo wa kampeni unatoa ramani- inayoelezea kauli mbiu, utangulizi wa kihistoria wa Siku 16, na kwa nini **mustakabali wa ufeministi** lazima kuutafakari, kuujenga, na kuulinda kwa pamoja.

Mwaka huu, pia tunatambua:

- Kumomonyoka kwa ufadhili wa umma kwa ajili ya utetezi wa haki za kijinsia na Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake
- Ukosefu wa uwajibikaji katika kuzuia ukatili unaowezeshwa na teknolojia
- Hitaji la haraka la kutoa majibu endelevu na mtambuka ambayo yanajumuisha usalama wa kidijitali, afya ya akili na haki za kiuchumi
- Kuongezeka kwa hatua za kupinga haki ambazo zinapinga kikamilifu usawa wa kijinsia, ambazo maelezo yake yanataka kurudisha nyuma faida zilizopatikana kwa jitihada kubwa juu ya haki na uhuru wa wanawake.

4.1 Muhtasari wa Kampeni

Waraka huu wa msingi unaonyesha ujumbe na malengo ya msingi ya kampeni ya mwaka huu. Itumie kuoanisha shughuli na mazungumzo yako katika maono mapana zaidi. Chapisha. Shiriki. Ubebe.

1. Zingatia Nguvu ya Alama: Vaa Utepe Wako

Kampeni ya kikanda ya Siku 16 za Uanaharakati Mwaka Huu itatumia, **Utepe wa Zambarau na Mweupe** kuashiria mshikamano wetu na wahanga, kujitoa kwetu kwaajili ya haki, na kukataa kwa pamoja kuhalalisha ukatili dhidi ya wanawake **katika aina zake zote**, ikijumuisha zile zinazofanyika kwenye runinga zetu.

Vaa Ribbon yako:

- Kutambua na kufahamu kwamba ukatili dhidi ya wanawake ni ukiukwaji wa haki za binadamu na kunahaja ya kuuzuia
- Mtandao wa Kuzuia UWAKI unatumia utepe mweupe kama ishara ya amani, kutokuwa na ukatili na mshikamano katika kukomesha ukatili dhidi ya wanawake. Halikadhalika utepe wa zambarau unatumika sana katika kampeni za kimataifa za kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake, ina uhusiano wa kina na maombolezo ya Mauaji ya Kimbari dhidi ya Watutsi nchini Rwanda na eneo la Maziwa Makuu. Ili kuheshimu muktadha huu wa kitamaduni, Mtandao ulichagua utepe mweupe kama ishara inayofaa zaidi kutuunganisha.
- Kama ishara ya matumaini, mawazo mapya na uwezekano wa kutengeneza maisha bora ya baadaye.
- Katika kupinga ufadhili mdogo unaotelelezwa kwa kipindi cha muda mrefu kwaajili ya huduma za uokozi wa maisha
- Kwa mshikamano na watetezi wa haki za wanawake wanaodhiriwa na ukatili wa kidijitali
- Kama ishara ya upinzani unaotaka kuturudisha nyuma



4.2 Anzisha fikra za kina na majadiliano ya Mabango ya Watetezi wa Haki za Kifeministi

Mabango yetu ya kampeni ni ya kijasiri, matamko ya bayana yanayo pinga na kufikiria upya. **Yanazingatia haki ya kupata ufadhili, usalama wa kidijitali, na mshikamano wa kifeministi.**

Mawazo unayoweza Kutumia:

- Andaa **Mduara wa Tafakari** ya Bango na maswali haya yaliyoongezwa:
 - o Je, Ukatili wa kidijitali una athari gani katika jamii yako?
 - o Je, tunawezaje kuwalinda walio hatarini zaidi mtandaoni?
 - o Tunaweza kufanya nini katika wakati huu tunaposhuhudia kupungua kwa ufadhili kunakotishia mifumo yetu ya usalama?
- Tuma kwenye mijadala ya mtandaoni, hasa katika nafasi za kidijitali—ofisini, sokoni, ofisi za serikali, vikundi vya kijamii vya WhatsApp, vituo vya Telegramu au akaunti za mitandao ya kijamii.

4.3. Sehemu za Maongezi ya Kifeministi: Anzisha Mazungumzo yenye Umuhimu

Mazungumzo ni mojawapo ya zana zenye nguvu zaidi tulizo nazo kwenye harakati za ufeministi. Ni namna tunavyotamka madhara, kushirikishana na walionusurika, kupeana hekima, na kuamsha ari katika kuchukua hatua ili kukuza maono ya pamoja. Katika wakati ambapo nafasi za watetezi wa haki za ufeministi ziko kwenye tishio kutokana na kupungua kwa ufadhili kwenye masuala ya ukatili wa kidijitali kunakosababisha na kukata tamaa—kuunda nafasi za makusudi za mazungumzo ni muhimu zaidi kuliko hapo awali.

Mistari ya Majadiliano ya Kifeministi imejumuishwa kwenye kiti ya mwaka huu imeandaliwa ili kuvunja ukimya, kuibua uakisi na kuongeza uelewa wa pamoja. Kila mistari unabeba swali, nukuu, au tafakari ya haraka ili kufungua mazungumzo ya kweli, kuhusu dunia tunaoishi—na mustakabali ujao ambao tuna ufikiria kwa upya.

Hii sio kuvunja ukimya. Hii ni kuvunja ukweli—ni vipande vidogo vya karatasi vyenye uwezo wa kuamsha ujasiri, mshikamano, na uelewa wa pamoja.

Vinaweza kutumika kwa njia nyingine nyingi:

- **Miduara na Mikusanyiko:** Waombe wazunguuke katika kikundi na kila mmoja ajibu. mistari moja, kwa kusimulia hadithi nyingi.
- **Mazungumzo ya ana kwa ana :** Yatumie kwenye kahawa, matembezini, wakati wa mapumziko ya chakula cha mchana. Acha maswali yaongeze muunganiko wako.
- **Nafasi za Mtandaoni:** Shiriki Mistari ya kidijitali na ualike majibu ya maandishi au video kutoka kwenye jamii yako.
- **Warsha au Matukio:** Zitumie wakati wa kufungua vikao, katikati ya mijadala, au kama tafakari wakati wa kufunga.
- **Nafasi za Uponyaji na Usaidizi:** Baadhi ya mazungumzo ni nyeti. Ruhusu mistari iongoze mazungumzo yaliyo nyeti kati ya marika, waathirika, au watoa huduma.





Katika kipindi cha ongezeko la uhalifu wa kidijitali, mistari hii pia inatoa mapumziko ya makusudi—kurejesha sauti na uwepo wa binadamu. Wanatukumbusha kwamba kujenga mustakabali wa utetezi wa haki za ufeministi haianzi kwa njia ya hati za mkakati au lebo za reli pekee—huanza na majadiliano ya kijasiri.

Iweke kwenye dawati lako. Katika mfuko wako. Kwenye meza yako ya jikoni. lache isafiri. lulize. Wacha wafungue kinachotakiwa kusemwa. Kwa sababu kila wakati ujao wa kifeministi tunaofikiria utajengwa—mazungumzo ya aina moja yenye uaminifu kwa wakati mmoja.

4.4. Kadi za Uthibitisho: Dai tena Kila Mwezi kwa Mamlaka

Sasa zaidi ya hapo awali, **uthibitisho wa kila siku ni mapambano.**

Wako hapa kukukumbusha mamlaka yako, kusudi lako, na nafasi yako katika jambo kubwa zaidi.

Hasa katika siku ambazo:

- Rasilimali zinakuwa katika hali ya uhaba, na kazi inazidi kuwa ngumu kuliko inavyotarajiwa
- Nafasi za mtandaoni zinakuwa katika misukosuko au zisizo na hali ya kuridhisha
- Taasisi zinaonekana kuwa mbali, hazina mwitikio, au zinabadilika polepole

Kila mwezi hauthibitishi tu thamani yetu, lakini haki yetu ya kustawi hata pale mifumo inapotukwamisha.

4.5. Sumaku za Jokofu

Tumia sumaku ya Jokofu kutaja shida na kudai mustakabali wa siku zijazo. Unaweza kuweka sumaku kwenye nyuso za metali katika ofisi au nyumbani kwako ili kuzionyesha na kuongoza uakisi.

Kwenye **sumaku ya mwaka huu utapata ujumbe ufuatao:**

- **Linda Nafasi ya Ufeministi—Mtandaoni na Nje ya Mtandao.**
- Mshikamano huanza kwa kujijali.
- Nguvu zetu huishi katika udada wetu

5. Tengeneza Hatua Utakazo Zichukua Mwenyewe

Kufikiria upya mustakabali wa Kifeministi kunamaana ya kutambua kuwa uanaharakati hauonekani katika namna sawa kila wakati na kwamba haupaswi kuwa hivyo. Kwa mtu binafsi, iwe ni sehemu ya shirika, au umeunganishwa kwenye vuguvugu kubwa zaidi, muktadha wako ni muhimu, na mchango wako ni wa muhimu.

Mwaka huu, tunakualika uandae hatua utakazo chukua zinazoakisi uhalisia wako na udai tena mamlaka yako hasa katika kipindi cha kupungua kwa nafasi, rasilimali, madhara ya kidijitali na uchovu unaosababishwa na migogoro.]

Kwa sababu ili kuimarika katika mshikamano na kustawi baada ya migogoro, ni lazima tuchukue umiliki wa nafasi zetu, zana na masimulizi.



5.1 Watu Binafsi: Kudai tena Mamlaka kwa Njia ya unyenyekevu, katika msimamo mkali

Hata katika kutengwa, sauti na uzoefu wako ni sehemu ya ushiriki wa pamoja. Hatua zako unazochukua zitakazo wafikia wengi.

- Shirikisha vidokezo vyako vya usalama wa kidijitali au andaa manifesto yako kwa ajili ya utu wako na ustahimilivu mtandaoni kwa sababu ya kufikiria upya mustakabali wa utetezi wa haki za kifeministi ni pamoja na kulindana katika nafasi pepe.
- Andika barua au barua pepe kwa wawakilishi wako katika jamii, Bunge, Seneti na Wawakilishi katika serikali za mitaa ukiwashinikiza kuweka kipaumbele kwenye ufadhili wa haki za kijinsia na utatuzi wa masuala ya kijamii. Shirikisha kwa nini rasilimali hizi ni muhimu kwako na kwa jamii yako, na kwa jinsi gani msaada unavyoweza kusaidia watu wote kustawi.
- Iwapo umekabiliana na aina yoyote ya ukatili, ikiwa pamoja na matumizi mabaya ya mtandaoni, ripoti na kuweka kumbukumbu za unyanyasaji wa kidijitali. Hauko peke yako, njia ya kuwa muwazi na kutoa taarifa ni sehemu ya uponyaji na kupinga.

5.2 Mashirika: Kuendeleza Kazi Inayoleta uendelevu wetu

Mashirika ya kifeministi ndiyo mapigo ya moyo ya vuguvugu hili—lakini wengi wanaombwa kufanya zaidi kwa kile kidogo walichonacho. Hebu turudi nyuma tutafakari—na tusonge mbele.

- Andaa Warsha inayohusu Usalama na Ustahimilivu Kidijitali ambayo itaonyesha hali halisi ya wanaharakati, wanahabari, vijana na walionusurika kutokana na vitisho mtandaoni.
 - Zindua kampeni ya kijasiri, isiyo ya kuomba msamaha inayoitaka bajeti ya umma inayolinda huduma za kifeminist kwa sababu Kazi ya Kuzuia, na kukabiliana na migogoro ni lazima ifadhiliwe, bila kusahaulika.
 - Shirikiana na wadau wenye ujuzi wa teknolojia na mashirika ya kutetea haki za kidijitali ili kuandaa suluhisho la pamoja la kusaidia wahanga na kulinda nafasi za kidijitali zinazotetea haki za kifeministi
 - Kuanzisha huduma ya kujijali kibinafsi na kwa pamoja katika kazi yetu ya kuhamasisha uponyaji na kuzuia kukata tamaa.
- 



5.3 Jamii: Kujenga Mustakabali wa Siku Zijazo kwa Pamoja

Nguvu yetu iko katika mshikamano wetu. Ili kufanikiwa kutoka kwenye migogoro, ni lazima tujitokeze kwa ajili ya kila mmoja wetu mtandaoni na nje ya mtandao huku tukisimamia nafasi ya kuonyesha changamoto kadhaa tunazokabiliana nazo: kupungua kwa rasilimali, kuongezeka kwa madhara ya kidijitali, na hasara ya kutiwa mkono kwa muda mrefu sana.

- Andaa mazungumzo katika jamii au nafasi za kujifunzia ambazo watu wanaweza kushirikishana uzoefu na zana za kuzuia vurugu za kidijitali, kuelewa faragha, na kudai tena hali ya kujitambua na usalama mtandaoni. Nafasi hizi zinaweza kutoa maarifa ya vitendo na msaada wa kihisia.
- Fanya uchunguzi wa pamoja kutambua ni teknolojia au majukwaa yapi yanayosaidia jamii yako na yapi yanasababisha madhara. Tumia taarifa hii kama chanzo cha kujenga uelewa wa kidijitali, fikiria njia mbadala zilizo bora, na fanya utetezi kuhusu teknolojia iliyo salama na inayowajibika zaidi.
- Andaa kitendo kitakachotoa mwonekano wenye utulivu lakini chenye nguvu zaidi kama vile maandamano ya “Toa Ufadhili kwa Wakati Ujao”, tengeneza sanaa, au mduara wa kusimulia hadithi ambao utaalika wengine waunge mkono mwito wa kuwekeza katika huduma zinazowaruhusu wanawake, wasichana na watu wa jinsia tofauti si kwa ajili ya kuishi tu, bali kuwa na ndoto, kujifunza, kuponya na kustawi.

Kila kitendo, hata kiwe kidogo namna gani, kinachangia kwenye siku zijazo tunazozijenga kwa pamoja.

Tunapofanya kwa nia moja, tunabadilisha utamaduni. Tunapoinuka katika mshikamano, tunakuza nguvu za kila mmoja. Tunapofikiria kwa ujasiri na kujipanga kwa kina, tunakumbusha dunia: Kesho iliyo bora si tu inawezekani. Tayari iko kwenye mwendo.

